HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO

Wah. Wajumbe,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Wilaya,
BAGAMOYO.

YAH: TAARIFA YA UFUNGAJI WA HESABU ZA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Wah. Wajumbe, Baraza la Madiwani, Ifuatayo ni taarifa ya ufungaji wa hesabu za mwaka wa fedha 2016/2017

1.0. UTANGULIZI:

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imeandaa hesabu za mwisho kwa mwaka 2016/2017. Hesabu hizi zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa kwa hesabu za sekta ya Umma (International Public Sector Accounting Standard – IPSAS) na Miongozo mbalimbali inayotolewa na TAMISEMI.

Kwa ujumla hesabu za mwaka 2016/2017 zimejumuisha fedha zinazotokana na vyanzo vya ndani, Ruzuku toka serikali kuu kwa ajili ya mishahara, Matumizi ya kawaida na fedha kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Kwa ujumla viwango vya kimataifa vinatamka kila Afisa Masuhuli kutengeneza Mahesabu yaani **"Financial Statement"** katika makundi kama ifuatavyo:-

01: Mizania (Statement of Financial Position)

02: Mapato na Matumizi (Statement of Financial Performance)

03: Taarifa ya mabadiliko katika mali (Statement of changes in Net equity)

04: Mtiririko wa fedha (Cashflow Statement)

05: Taarifa ya Uongozi (Councillors/Board of Directors report)

2.0. MAPATO:

2.1. MAPATO YA NDANI:

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilikisia kukusanya jumla ya **Tshs. 2,801,539,000/=** kutokana na vyanzo vya ndani. Hadi kufikia 30 Juni 2017 Halmashauri ilikuwa imefanikiwa kukusanya jumla ya **Tshs. 2,614,290,645/=** ikiwa ni sawa na **asilimia 93%** ya makisio ya **Tshs. 2,801,539,000/=.**

2.2. RUZUKU MBALIMBALI:

Kwa mwaka **2016/2017** jumla ya **Tshs. 41,398,084,059/=** zilikisiwa kukusanywa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kulipia mishahara na Matumizi ya Mengineyo na miradi ya maendeleo. Hadi Juni, 2017 jumla ya **Tshs. 26,017,973,744/=** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara na Matumizi mengineyo na **Tshs. 4,698,247,820/=** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hivyo Ruzuku kwa ujumla zilipokelewa jumla ya **Tshs. 30,716,221,563/=** ikiwa ni sawa na **asilimia 74.2%** ya makisio ya **Tshs. 41,398,084,059/=.**

2.3. MIRADI YA MAENDELEO:

Jumla ya Tshs. **9,761,827,933/=** zilikisiwa kwa mwaka 2016/2017 kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Hadi Juni, 2017 jumla ya Tshs **4,698,247,820/=** zilipokelewa toka Serikali Kuu, Wahisani na vyanzo vya ndani hii ni sawa na asilimia **48%** ya makisio ya Tshs **9,761,827,933** Fedha hizi zilizopokelewa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya:-

NA	JINA LA MRADI	KIASI (TSHS)
1	EGPAF – FUND	6,071,598
2	TASAF – NATIONAL VILLAGE	2,916,270,015
3	RWSSP	392,840,204
4	DADP/ASDP	0
5	ROAD FUND	836,040,111
6	MFUKO WA JIMBO: BAGAMOYO	29,749,000
7	EDUCATION FUND: SECONDARY – SEDP	0
8	MFUKO WA AFYA	202,220,000
9	N.T.D. FUND	23,922,100
10	THPS	110,263,453
11	PFM	10,958,339
12	MIVARAF	22,000,000
14	LGCDG	147,913,000
	JUMLA TSHS	**4,698,247,820**

HESABU ZA KATA, SHULE NA VITUO VYA HUDUMA ZA AFYA:

Kwa mwaka 2016/2017 Hesabu za Halmashauri ya wilaya Bagamoyo zimejumuisha taarifa za Mapato na matumizi ngazi ya Kata, Shule za Sekondari na Msingi pamoja na Vituo vya kutolea Huduma za Afya vya Wilaya.

3.0. WADAIWA NA WADAI WA HALMASHAURI

3.1. WADAIWA WA HALMASHAURI:

Jumla ya Tshs. **1,108,472,459** ni fedha ambazo Halmashauri ya wilaya Bagamoyo inadai fedha toka maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

NA	. JINA LA MDAIWA	KIASI (TSHS)	MAELEZO
1	Wizara ya Fedha (Hazina)	201,880,436	Hizi ni fedha ambazo watumishi wanadai kutoka Hazina ambazo wanastahili kulipwa kulingana na stahili zao.
2	Adosta Investment Ltd	129,805,000	Hizi ni fedha anazodaiwa wakala wa mapato (misitu). Ambapo hukumu imetolewa na Halmashauri imeshinda kesi (Deni hili ni pamoja na riba).
3	Vikundi vya Akina Mama na Vijana	248,660,389	Fedha hizi zimekopeshwa kwa vikundi vya Akina Mama na Vijana
4	Watumishi	6,018,950	Fedha hizi ni masurufu kwa watumishi mbalimbali kuishia Juni, 2017
5	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	357,289,093	Asilimia 30% Kodi ya ardhi kutokana na fedha ziliyowasilishwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hadi Juni, 2017.
6	Wizara ya Fedha (Hazina)	164,818,591	Fedha za Madawa toka Wizara ya Afya kwenda bohari ya Madawa-MSD
	JUMLA TSHS	**1,108,472,459**	

3.2. WADAI WA HALMASHAURI:

Jumla ya **Tshs.1,629,196,814** ni madeni mbalimbali ambayo Halmashauri inadaiwa na watu mbalimbali kama ifuatavyo:-

NA	WADAI	KIASI	MAELEZO
1	M/S Mzinga Holding Co. Ltd.	466,767,579	Deni la ujenzi wa maabara saba(7)shule za Sekondari kwa Halmashauri ya wilaya Bagamoyo.
2	Watumishi (Unclaimed Salaries)	56,732,253	Mishahara ya watumishi ambayo imezuiliwa kutokana na sababu mbalimbali kama utoro, kustafu au kukosa sifa za kuwa mtumishi. (Unclaimed Salaries)
3	Wazabuni	5,376,470	Madeni ya wazabuni yaliyo kwenye ngazi ya mkataba wa kutoa huduma.(LPO).
4	Mfuko wa TASAF	40,918,927	Fedha za Mfuko wa TASAF,
5	Wizara ya Sheria	916	Fedha zilizobaki zoezi la Katiba
6	Watumishi	201,880,436	Haya ni madai ya watumishi toka Hazina na mapato ya ndani ambao wanastahili kulipwa kutokana na stahili zao.
7	Fidia Mbalimbali za Ardhi	269,855,182	Fidia mbalimbali za ardhi kwa ajili ya kulipa wananchi
8	Wizara ya Fedha (Hazina)	275,000	Fedha za mahindi ya njaa
10	Marejesho mikopo (Revolving Funds)	117,040,124	Fedha hizi ni fedha kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Wanawake/Vijana
11	Wizara ya Fedha na Mipango	71,517	Fedha zilizobakia wakati wa zoezi la Sensa ya watu na makazi